# JARIDA LA KILIMO HIFADHI

MACHI 2023 ● UJAZO NAMBA 9 ● NAKALA YA 1

**NDANI YA TOLEO HILI**

Kilimo Hifadhi Katika Mazingira ya Mvua
Vidokezo vya Kusimulia Hadithi kwa Ufanisi
Wasifu wa Mkulima wa Kilimo Hifadhi: Chrissie Stackio, Malawi
Wasifu wa Mshirika: Kanisa la Ndugu katika Kristo
Ratiba ya Ziara za ALTA

## Kilimo Hifadhi Katika Mazingira ya Mvua



Eunice Mwalimba Wanyeta (kulia) katika shamba lake la kilimo hifadhi na nyuma ya mahindi ya kawaida

***Neil Rowe Miller, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha kwa Afrika Mashariki***

Eunice Mwalimba Wanyeta, mkulima kiongozi katika mradi wa CARD huko Mulanje, Malawi, amekuwa akitumia Kilimo Hifadhi (KH) kwenye mashamba madogo kwa miaka minne. Ardhi yake iko katika sehemu ya chini inayokabiliwa na mafuriko, na kwenye mashamba yake ya kawaida yeye hupanda kwenye matuta ili kuzuia maji kutoweka. Tulipomtembelea mwezi Februari, mahindi yake ya kawaida yalionekana kuwa na afya zaidi kuliko shamba lake la Kilimo hifadhi, ambalo lilipandwa kwenye udongo tambarare badala ya matuta. katika shamba la kilimo hifadhi uotaji ulikuwa duni, na alilazimika kupanda tena kwenye mapengo.


Mbinu za kilimo hifadhi zinaweza kuongeza kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa maji kwenye udongo kwa kuongeza upenyezaji na kupunguza uvukizi. Katika mazingira kame hii inaweza kusababisha ongezeko kubwa la mavuno. Ingawaje katika mazingira yenye unyevunyevu, ongezeko la maji mengi inaweza kusababisha matatizo kama yale yanayompata Eunice.

Wakati kannuni za Kilimo hifadhi za kupunguza usumbufu katika udongo, kuongeza matumizi ya mafunika ardhi na kuchanganya mazao mbalimbali zinaeleweka kwa wote; utendaji kazi wa kilimo hifadhi unahitaji kubadilika kulingana na kila mazingira ya kilimo-ikolojia. Wakati sehemu kubwa kusini mwa jangwa la Sahara kule Afrika inakabiliwa na uhaba wa mvua, baadhi ya maeneo yanapata mvua za kutosha kiasi kwamba kukatika kwa maji

Canadian Foodgrains Bank
A Christian Response to Hunger

**Washauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha wa Canadian Foodgrains Bank**

**John Mbae** john.mbae@tearfund.org
**Neil Rowe Miller** neil.rowe-miller@tearfund.org
**Jean Twilingiyumukiza** jean.twilingiyumukiza@tearfund.org
**Lilian Zheke** lilian.zheke@tearfund.org




**Hata kiasi kidogo cha kifuniko cha udongo, kinaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa momonyoko wa udongo (kutoka Nill, D. et al., 1996 ndani ya Soil Erosion by Water in Africa.**

wakati mwingine unaharibu mazao. Katika mazingira haya, utendaji kazi wa kilimo hifadhi unahitajika kupokelewa.

## KIASI GANI CHA MAFUNIKA ARDHI YATATOSHA KUNUFAISHA UDONGO?

Katika mazingira kame wakulima wanapaswa kuongeza kiwango cha juu cha kufunika udongo kwa kutumia mabaki ya mazao, mazao ya kufunika au matandazo. Mbali na kuboresha uhifadhi wa maji, mafunika ardhi hupunguza mmomonyoko wa udongo, huongeza shughuli za kibiolojia, na hutoa makazi kwa wadudu wenye manufaa. Katika mazingira yenye unyevunyevu, wakulima wa kilimo hifadhi watahitaji kupunguza kiasi cha mafunika ardhi, hasa katika hatua za awali za ukuaji wa mmea.

Wakulima wa Kilimo hifadhi katika eneo lenye mvua nyingi nchini Burundi, kwa mfano, huondoa mabaki katika sehemu za kupanda wakati wa kupanda na kuyaacha katikati ya safu. Wakati na baada ya palizi ya kwanza, wakati mimea imeimarishwa vizuri, hurudisha mabaki kwenye safu, na kuongeza matandazo ya ziada yanapopatikana. Njia hii huwasaidia kuepuka matatizo ya kuchipua, lakini huilinda dhidi ya vipindi vya kiangazi vya msimu wa baadaye.



**Matuta ya kudumu (derdero) chini ya CA nchini Ethiopia**

Je, ni kwa kiasi gani wakulima wanaweza kupunguza kufunika udongo na bado wakafaidika na faida kama vile mmomonyoko wa udongo? Tafiti nyingi katika bara hili zimeonyesha kuwa kiasi kidogo cha asilimia 30 ya mafunika ardhi yanaaweza kupunguza mmomonyoko wa ardhi mpaka asilimia10 tu ya ule kwenye ardhi tupu. Kwa sababu hii, katika mazingira yenye unyevunyevu, wakulima bado wanapaswa kudumisha udongo, ingawa ni chini ya asilimia 100.

## MATUTA YALIYOINULIWA YA KUDUMU KWA AJILI YA KUONDOA MAJI –

Suluhisho lingine la kutumia kilimo hifadhi katika maeneo yenye unyevunyevu ni kupanda mimea kwenye matuta yalioinulinuliwa ili unyevu uliopitiliza uondoke. Kwenye udongo wenye maji mengi, mimea haipati oksijeni, lakini kwa kuinua hayo matuta yataruhusu oksijeni kupitia mizizi. Zaidi ya hayo, katika udongo uliojaa maji, naitrojeni ipatikanayo kwa mimea haibadilishwi (inabadilishwa kuwa mfumo usiyopatikana katika mimea) hivyo mifereji bora ya maji inaweza pia kupunguza upotevu wa nitrojeni.



**Matuta yalioinuliwa ya Kudumu (*imitabo*) chini ya kilimo hifadhi nchini Rwanda**

Mifumo mingi ya kilimo cha kitamaduni ni pamoja na aina fulani ya matuta yaliyoinuliwa au mitaro. Hata hivyo, mara nyingi miundo hii inachimbwa tena kila mwaka kukiuka kanuni ya msingi ya kilimo hifadhi ya kupunguza usumbufu wa udongo. Miradi ya kilimo hifadhi nchini Rwanda na Ethiopia imekubali matumizi ya matuta ya

kitamaduni yaliyoinuliwa, lakini wanahamasisha kuyafanya kuwa ya kudumu badala ya kuyajenga upya kila mwaka. Kwa njia hii, wananufaika kutokana na kuboreshwa kwa mifereji ya maji ya matuta wakati wa misimu wa mvua, lakini pia wananufaika kutokana na kufunika udongo wakati wa kiangazi. Miundo ya matuta ya kudumu yalioinuliwa pia hupunguza kazi inayohitajika kuchimba tena kila mwaka.

## Vidokezo vya Kusimulia Hadithi kwa Ufanisi

***Christina Philips, Meneja Mawasiliano wa Foodgrains Bank***

Utekelezaji bora wa miradi ya kilimo na maisha ni hatua ya kwanza tu katika kuhakikisha usalama wa chakula endelevu. Kuwasilisha mafanikio yako kwa washirika, maafisa wa serikali na washikadau wengine kutasaidia sana kuhakikisha kwamba juhudi zako zinaendelea kuitumikia jamii yako katika siku zijazo. Hapa kuna vidokezo vya kukusaidia kusimulia hadithi yako kwa ufanisi:



*Nchini Ethiopia, Meserat anashiriki mafanikio yake na kilimo cha CA kama vile Bereket kutoka TDA anavyotafsiri Andy kutoka Foodgrains Bank.*

### KUANDAA MAHOJIANO

- ***Kuwa mwangalifu kwamba katika kusimulia hadithi hakutamuweka mtu yeyote hatarini***. Ikiwa unahitaji kuwahakikishia usalama wao, badilisha jina la mshiriki na utumie maeneo ya jumla ya kijiografia.
- ***Je, mtu huyo yuko kwenye hali ya utulivu?*** Fuata kanuni zao za kitamaduni ili wawe na raha na wajue kuwa wanaheshimiwa. Wakati watu wanautulivu, wana uwezekano mkubwa wa kushirikisha.
- ***Eleza kwa nini unakusanya hadithi na kwamba hadithi yao ni muhimu!*** Wajulishe kuwa picha au video zao zinaweza kutumika katika vipeperushi, mitandao ya kijamii, vijarida vya kuchapisha na zaidi.
- ***Omba idhin*. ** Mara tu wanapoelewa jinsi gani hadithi yao inaweza kutumika, waulize waamue kama wangependa kushiriki. Pata ruhusa kwa maandishi, kwa maneno au kwa video. Kitendo hiki kinawapa nguvu, na kuwafahamisha kuwa hadithi yao ni yao wenyewe.
- ***Toa msaada unapohitajika*.** Baadhi ya washiriki wa mradi wanaweza kuchochewa au kuumizwa tena wakati wanasimulia hadithi zao. Ikiwa mshiriki anakasirika, muulize kama angependa kupumzika. Kuwa na mwanafamilia, jirani, au mtu mwingine wa msaada wa kihisia kunaweza kusaidia.

## FANYA MAHOJIANO

Usahihi ni heshima. Mahali pazuri pa kuanzia kunasa taarifa muhimu ni kwa kuuliza nani, nini, lini, wapi, kwa nini na vipi.

- ***Nani anahusika?*** Nasa maelezo muhimu kuhusu mtu huyo: jina, umri, jinsia, kazi au kiwango cha daraja, na mahusiano ya kifamilia. Eleza jinsi wanavyosikika au jinsi wanavyoonekana wanapozungumza.
- ***Nini kinaendelea?*** Tambua ni matukio gani muhimu yamefanyika. Ni nini kilibadilika katika maisha yao? (mafunzo, vikundi vya kuweka akiba n.k.) Ikiwa tunazungumzia kuhusu mavuno ya mazao, walikuwa na kiasi gani hapo awali ikilinganishwa na sasa? Ni nini kimesababisha mafanikio yao? Changamoto zao ni zipi?
- ***Hii ilitokea lini?*** Muda unaofaa unaweza kutoa muktadha. Kulikuwa na mafuriko/ukame/mvua ya mawe - lini? Je, kuna athari za msimu? Je, mshiriki amepitia mafanikio fulani au amekumbana na changamoto kwa muda gani?
- ***Hii ilifanyika wapi?*** Jumuisha mahali ambapo mshiriki anaishi na kufanya kazi. Eleza mpangilio na maelezo yoyote muhimu ambayo husaidia kuweka mandhari kwa ajili ya hadhira. Kumbuka kwamba watazamaji pengine hawajawahi kutembelea eneo hilo.
- ***Kwa nini hili lilitokea?*** Toa muktadha unaozunguka hadithi ya mshiriki. Je, 'kabla' ilikuwaje? Kwa nini walishiriki katika mpango fulani? Je, kuna maelezo ya kihistoria, kitamaduni au kikanda ambayo yamesababisha hali ya sasa?
- ***Je, hii inafanyikaje?*** Eleza jinsi mshiriki anavyobadilisha maisha yao. Hii inaweza kujumuisha jinsi wanavyotunza familia zao na jinsi wanavyofanya kazi ili kupata usalama wa chakula.

### Vidokezo zaidi vya kupata majibu ya kina katika mahojiano:

**ULIZA MASWALI WAZI AMBAYO YATALETA MAJIBU ZAIDI YA 'NDIYO' AU 'HAPANA.'**

"Umejifunza nini kupitia uzoefu huu?"

**ULIZA MASWALI YA UFUATILIAJI AMBAYO YANAMPA MHOJIWA FURSA YA KUTAFSIRI UZOEFU WAO WENYEWE.**

"Ni nini kimekuvutia zaidi?"

**ULIZA KAMA MSHIRIKI ANGEPENDA KUSHIRIKISHA JAMBO LOLOTE AMBALO HALIJAJADILIWA.**

"Je, kuna kitu kingine chochote ungependa kuongeza?"

**Nukuu za moja kwa moja.** Usifungue maneno au kuongeza maneno ya kiufundi. Badala yake, ripoti nukuu zao kama zinavyosemwa.

## KUANDIKA HADITHI

Hadithi moja ni muono tu wa mtu mwenye sura nyingi na maisha kamili. Kadiri unavyotoa maelezo zaidi kuhusu utu wao, maisha yao, na hadithi zao; ndivyo unavyotoa picha kamili.

- ***Mapambano ya mtu hayambainishi mtu*.** Eleza hali zao ngumu, lakini usitumie vibaya. Mshiriki ni shujaa kwa sababu walichagua kushiriki na wanachukua hatua kufikia usalama wa chakula.
- ***Ni nini kinachomfanya mtu huyu kuwa maalum kwako?*** Unapoandika kutoka moyoni, hadithi yako itavutia zaidi mioyo ya msomaji.

| MAMBO YA KUFANYA NA AMBAYO SI YA KUFANYA WAKATI WA KUSIMULIA HADITHI KWA HESHIMA | |
|---|---|
| **FANYA** | **USIFANYE** |
| Onyesha mshiriki wa mradi kama shujaa katika maisha yao wenyewe. | Fanya shirika la ufadhili kuwa shujaa wa hadithi. |
| Toa habari ya historia na muktadha wa mshiriki ili msomaji awe na wazo nzuri la kile kinachotokea. | Chukulia hadhira yako inajua historia na muktadha wa kitamaduni wa hadithi. |
| Jumuisha nukuu za moja kwa moja za washiriki na ukweli unajieleza wenyewe. | Fafanua hadithi au ujumuishe tafsiri zako mwenyewe. |
| Jadili sababu tofauti na sababu tata kwa nini mtu anaweza kukabiliwa na njaa. | Rahisisha kupita kiasi masuala magumu. |
| Uliza maswali ya kufuatilia au fafanua habari na mhojiwa wako. | Jaza mapengo kulingana na uzoefu wako mwenyewe au uelewa wako wa mahojiano. |
| Onyesha chanya sambamba na hasi. | Kuzingatia tu upande mbaya. |
| Shiriki malengo na ndoto za mshiriki kwa siku zijazo. | Onyesha mradi kama mafanikio ya mwisho katika maisha ya mshiriki. |
| Jaribu na uonyeshe utu wa mshiriki. (Je, wana furaha, huzuni, msisimko, au hasira?) | Onyesha mtu huyo kana kwamba ni sawa na mtu mwingine yeyote katika jamii yake. |
| Hebu moyo wako usogezwe na mtu huyu | Mtazame mtu huyu kama kitu - wameumbwa kwa mfano wa Mungu. |




**Kikundi cha wakulima wakuu huko Chambo, Malawi.**

# Wasifu wa Mkulima wa Kilimo Hifadhi: Chrissie Stackio, Malawi

Chrissie Stackio, mkulima mdogo kutoka Chambo, Malawi, alikuwa akilima ekari tatu na nusu za ardhi yake. Kwa ujumla ilizaa chini ya magunia saba ya kilo 50 ya mahindi. Kwa wengine, hii inaweza kuonekana kuwa nyingi, lakini kwa mama wa watoto sita asiye na mume anayejaribu kulisha familia yake, haikutosha. Na aliweza kumudu kupeleka watoto wawili tu shuleni.

Baadhi ya mikoa ya Malawi inakabiliwa na ukame unaoendelea, magonjwa ya mazao na mifugo na udongo ulioharibika. Matokeo? Familia kama za Chrissie, kuwa na wasiwasi mara kwa mara kama zitakuwa na chakula cha kutosha.

Mwanachama wa Benki ya nafaka za chakula jeshi la ukombozi (TSA) nchini Kanada inafanya kazi na jeshi la Ukombozi nchini Malawi kutekeleza mradi wa Kilimo Endelevu na Usalama wa Chakula (SAFS) katika Wilaya ya Mangochi. Mradi huo wa miaka mitatu unawapatia wakulima 450 na kaya zao (takriban watu 2,950) mafunzo ya kilimo hifadhi (KH). Mbinu za kilimo hifadhi zinaweza kusaidia kuongeza rutuba ya udongo, kuongeza uzalishaji wa chakula, na kujenga ustahimilivu katika mifumo ya ndani ya kilimo kwa kupunguza utifuaji wa udongo na kuchanganya mazao. Wakulima viongozi 30 wanahamasisha kilimo hifadhi katika jumuiya zao, na mafunzo ya SAFS ambayo yanajumuisha ufahamu wa usawa wa kijinsia.

Chrissie aliajiriwa kwa mradi wa SAFS, ambapo alifunzwa mbinu za kilimo hifadhi. Kuanzia na mashamba madogo mawili, alistaajabu alipovuna magunia 35 ya mahindi. "*Mungu amenifanyia njia," akasema kwa mshangao. "Matumaini yangu yalikuwa yametoweka lakini naona watoto wangu wanaweza kutabasamu tena."*

Alihifadhi magunia 15 kwa ajili ya chakula cha familia yake, ya kutosha kwa mwaka mzima, na akauza mifuko 20 na kuingiza MWK150,000 (C$195). Alitumia baadhi ya mapato kuwapeleka watoto wake wengine wanne shuleni, na akatunza baadhi kupitia ushirika wa Kuweka na Kukopa ya Kijiji.

Makala haya yalichapishwa awali katika toleo la *Winter 2023 edition of Breaking Bread.*

# Wasifu wa Mshirika: Kanisa la Ndugu katika Kristo - Huduma zenye Huruma kuleta Maendeleo (BICC - CODES), Malawi

***Lilian Zheke, Mshauri wa Kiufundi wa Kilimo na Maisha kwa Kusini mwa Afrika***



Wakulima waongoza mafunzo ya mbolea ya Mbeya

Huduma zenye huruma na kuleta .Maendeleo (CODES) ni mkono wa msaada na maendeleo wa Kanisa la ndugu katika Kristo (BICC) nchini Malawi, lililopewa jukumu la kuwafikia wahitaji, wasiojiweza na wanaokandamizwa; na kukuza mipango ya maendeleo. Maeneo ya kuzingatia ya shirika la CODES ni pamoja na: kuboresha usalama wa chakula, kudumisha ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya tabia nchi, na mwitikio unaolengwa kwa mahitaji ya dharura ya kibinadamu. BICC-CODES ni mshirika wa Benki ya Nafaka za chakula Kanada kupitia Kamati Kuu ya Wamennonite (MCC).

BICC-CODES kwa sasa inatekeleza mradi wa miaka mitatu wa usalama wa chakula unaofadhiliwa na CFGB/MCC. Mradi ulianza Aprili, 2021 na unakusudia kufikia kaya 400 katika Mamlaka ya Kimila ya Chikwawa. Mkakati wa mradi ni kuongeza uhakika wa chakula na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia Kilimo Hifadhi (KH), kuboresha upatikanaji wa soko na upatikanaji wa rasilimali fedha kupitia vikundi vya Akiba na Ukopeshaji vya Vijiji (VSLs). Mradi pia unatetea masuala ya jinsia, na jinsia inaingizwa katika vipengele vyote kwa lengo la kuongeza ushiriki na kufanya maamuzi ya wanawake. Ili kukuza uhifadhi wa maliasili, na pia kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake, mradi unadumisha majiko ya kupikia yenye ufanisi mkubwa. CODES hufanya kazi na wakulima viongozi wanaojitolea na mabingwa wa maswala ya jinsia ili kuongeza ufikiaji wao na vile vile kuwezesha kujifunza kutoka kwa rika hadi rika.



Shamba la KH chini ya mtama na zao la choroko

Ingawa kimbunga Ana kiliathiri washiriki wa mradi katika mwaka wa kwanza, matokeo makubwa tayari inaonekana katika eneo hilo. Wakulima wanashuhudia kwamba kilimo hifadhi hunufaisha uhifadhi wa unyevu wa udongo, hupunguza shinikizo la magugu na kuboresha vituo vya mazao. Mbinu za kilimo hifadhi pamoja na uhamasishaji wa mbegu zinazostahimili ukame na mbolea ya Mbeya zimechangia katika kuboresha kwa ujumla utendaji wa mazao. Utafiti wa serikali ya mavuno ya mwaka 2021/22 uliripoti wastani wa ongezeko la 67% ya mavuno ya mtama, ongezeko la 7% la mazao ya kunde na ongezeko la 9% la mavuno ya ufuta. Baadhi ya washiriki wa mradi wameongeza ukubwa wa maeneo yao ya  hadi kilimo hifadhi hekta 0.2-0.4 kwa matumaini ya kupata uzalishaji wa juu zaidi.

Ukuzaji wa usawa wa kijinsia na usawa umeachakuhamasisha kufanya maamuzi ya pamoja kwa shughuli za kaya. Familia huamua kwa pamoja mahali pa kulima na nini cha kukuza, jinsi ya kutumia mapato yanayopatikana, na jinsi ya kushiriki majukumu ya kaya. Kwa mfano, kwa sasa ni jambo la kawaida na linakubalika kwa waume kusaidia kupika, kuchota maji na kuni - mambo ambayo, miaka iliopita, yalikuwa mwiko kwa wanaume. Uhamasishaji wa majiko ya kupikia yenye ufanisi wa nishati umesaidia kuhifadhi maliasili kupunguza muda unaotumika kutafuta kuni. Wanawake sasa wana muda zaidi wa kushiriki katika shughuli za kilimo, kuhudhuria vikundi vya Akiba na Ukopeshaji vya Vijiji (VSLs) na mikutano mingine ya vikundi; na pia kuzingatia biashara ndogo ndogo.



**Bwana anamsaidia mke wake kupika, jukumu ambalo hangelifanya hapo awali**

# RATIBA YA ZIARA ZA ALTA

## Lilian Zheke

**24-29 April**
***Mazowe, Zimbabwe***
Warsha ya wakufunzi Bingwa wa kilimo hifadhi

**15-19 Mei, 2023**
***Masvingo, Zimbabwe***
Washiriki wa PAOZ na ZCC wanafanya ziara na mafunzo

**4-18 Juni, 2023**
***Winnipeg, Kanada***
Ziara za mipango mkakati na miradi inayoendelea kukua

**26- 30 Juni, 2023**
***Tete, Mozambique***
Ziara za washiriki wa CCM

## Jean Twilingiyumukiza:

**4-5 Aprili, 2023**
***Bugesera, Rwanda***
Warsha ya utetezi wa kilimo hifadhi zaidi

**17-21 April, 2023**
***Rwanda kaskazini***
Mafunzo ya kilimo hifadhi kwa wafanyakazi wa WFP & serikali

**1-6 Mei, 2023**
***Niamey, Niger***
Mafunzo ya wafanyakazi wa Samaritan's Purse

**7-12 Mei, 2023**
***Ouagadougou, Burkina Faso***
Kujenga timu kwa wafanyakazi wa ODE &MCC

**22-26 Mei, 2023**
***Kusini mwa Rwanda***
Mafunzo ya kuhuisha mkufunzi mkuu

**4-8 Juni, 2023**
***Rabat, Morocco***
Kongamano la 3 la kilimo hifadhi la Afrika

**9-16 Juni, 2023**
***Winnipeg, Canada***
Upangaji wa kimkakati na ziara za kukuza mradi

## John Kimathi Mbae

**3-4 Aprili, 2023**
***Kajiado, Kenya***
Ziara ya ushauri wa mkufunzi mkuu, MIDI & CITAM

**5-7 Aprili, 2023**
***Makueni, Kenya***
Ziara ya ushauri wa mkufunzi mkuu, serikali ya UDO

**8-9 Aprili, 2023**
***Turkana, Kenya***
Ziara ya ushauri wa mkufunzi mkuu, ADRA & NCM

**11-21 Aprili, 2023**
***Soroti & Kotido, Uganda***
Kutembelea miradi ya PAG na COU

**25-30 Mei, 2023**
***Addis Ababa, Ethiopia***
Mkutano wa uzinduzi wa NBS

**4-8 Juni, 2023**
***Rabat, Morocco***
Kongamano la 3 la kilimo hifadhi la Afrika

**9-16 Juni, 2023**
***Winnipeg, Canada***
Upangaji wa kimkakati wa ziara za kukuza mradi.

## Neil Rowe Miller

**11-21 Aprili, 2023**
***Uganda***
Kutembelea miradi ya PAG na COU

**1-5 Mei, 2023**
***Hanang, Tanzania***
Kutembelea mradi wa One World project.

**15-27 Mei, 2023**
***Ethiopia***
Kutembelea mradi na uzinduzi wa mkutano wa NBS

**4-13 Juni, 2023**
***Winnipeg, Canada***
Mipango ya kimkakati na ziara za wafadhili.